**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MVOMERO**

# HOTUBA YA MAADHISHO YA SIKU SHERIA NCHINI KUTOKA KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MVOMERO LEO TAREHE 6th FEBRUARI 2019.

**Imeandaliwa na:**
**Asha Hasan Waziri**
**Hakimu Mkazi Mfawidhi**
**Mahakama ya Wilaya Mvomero**

**Mheshimiwa: Mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero,**

**Mhe. Katibu Tawala wa Wilaya ya Mvomero,**

**Waheshimiwa Mahakimu wa ngazi zote,**

**Wanasheria wa Serikali/ Kujitegemea,**

**Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Mvomero,**

**Wahe. Madiwani,**

**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero,**

**Afisa Usalama wa Taifa Wilaya ya Mvomero,**

**Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mvomero,**

**Mkuu wa Gereza wa Wilaya ya Mvomero,**

**Mkuu wa Takukulu wa Wilaya ya Mvomero,**

**Afisa Utumishi Mahakama ya wilaya ya Mvomero,**

**Wakuu wa Idara,**

**Viongozi wa Dini,**

**Wanasiasa,**

**Viongozi wa Serikali za mitaa,**

**Tasisi za kibenki,**

**Wazee wa Baraza,**

**Wazee maarufu,**

**Watumishi wote wa Serikali na Mahakama ya Wilaya ya Mvomero.**

**Mabibi na Mabwana,**

**HOTUBA YA MAADHISHO YA SIKU YA SHERIA NCHINI**

**KUTOKA KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MVOMERO**

**LEO TAREHE 6TH FEBRUARY 2019.**

## UTANGULIZI.

Mheshimiwa mgeni rasmi, kwanza kabisa nichukulie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa ulinzi wake na kwa kutuwezesha kuuvuka mwaka na kutufikisha mwaka huu wa 21 na leo hii tupo hapa katika uwanja huu wa haki lengo kuu ikiwa ni kusherehekea siku ya sheria nchini.

Mheshimiwa mgeni rasmi, leo hii tunaadhimisha siku ya sheria nchini ambayo inaashiria kuanza mwaka mpya wa utendaji wa Mahakama, wanasheria na wananchi kw aujumla tunapata nafasi ya kujitathimini na kutathimini utendaji kazi wetu na kujitoa kwetu katika kutimiza wajibu wetu kwa mujibu wa sheriazetu na misingi ya bora ya demokrasia iliyotukuka. Na zaidi ya yote, maadhimisho haya yanalenga kutoa elimu, kukumbushana kila mmoja wetu kutekeleza wajibu wake kwa kutafakari maudhui yaliyochaguliwa na kuongelewa kwa mwaka husika. Hivyo basi wananchi na wadau mbalimbali wa mahakama kupata nafasi ya kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na mahakama. Kwa mwaka huu maudhui ya siku ya sheria yanayojadiliwa ni.

***"UTOAJI HAKI KWA WAKATI; WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU "***

Mheshimiwa mgeni rasmi, ili kuelezea vizuri maudhui haya nitaelezea maana ahalisi ya maneno yafuatayo; maneno hayo ni Haki, Tehama pamoja na Maadili.

## MAANA YA HAKI

Kwa kuanza nitaanza na neno Haki kwa tafsiri ya kamusi ya Kiswahili sanifu lina maana ya "jambo ambalo mtu anastahiki au kitu mtu anachostahili kuwa nacho. Kwa tafsiri ya kamusi ya kisheria neno haki lina maana ya kile mtu anachostahili kuwa nancho au kile anachoruhusiwa kufanya au kile anachostahili kupokea kutoka kwa wengine kwa mujibu wa sheria. Kwa tafsiri hii tunaweza kuona kuwa sheria ndio msingi wa haki. Sheria inasema kile unachostahili kuwa nacho, au unachoruhusiwa kufanya au kupata kutoka kwa wengine. Kwa maana pana zaidi tunaweza kusema haki ni maslahi ya mtu ambayo yanatambuliwa na na kulindwa na sheria.

Katika sheria zetu za Tanzania zipo haki mbalimbali zinazotambuliwa kwa mujibu w akatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Haki hizi zinafafanuliwa kupitia sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia na mamlaka nyingine zenye uwezo wa kutunga sheria. Mfano wa Haki hizo ni Haki ya usawa, haki ya kuishi, haki ya uhuru binafsi, haki ya kufanya kazi na haki ya kumiliki mali. Haki hizi mbalimbali utazipata sehemu ya tatu ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia, 1977 kuanzia ibara ya 12 – 32.

Mheshimiwa mgeni rasmi, mahakama ndio mhimili pekee uliyorasmishwa na kupewa mamlakana katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika utoaji haki. Kwa mujibu wa ibara ya 107A ya katiba hiyo. Ibara ya 107A (2) (a) (b) ya katiba inazitaka mahakama kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi na pia kutokuchelewesha haki bila ya sababu za msingi.

Hivyo basi kwa kuzingatia mamlaka haya iliyotunukiwa kikatiba, mahakama ndio muhimili peke wa kutoa huduma za haki ya kisheria kumlenga mwananchi ikishirikiana na taasisi nyingine za serikali, dini na binafsi. Mahakama kazi yake kubwa ni kutafsiri sheria ambazo zimetungwa na bunge la Jamhuri ya Tanznaia. Kuhakikisha haki inatendeka kwa wahusika wanaotafuta haki zao. Lakini pia mahakama inafanya kazi zake kwa ushirikiano wa karibu na asasi pamoja na taasisi mbalimbali za kijamii, serikali, binafsi na vyama ambavyo uhusika katika kutoa huduma za haki kumlenga mwananchi zikishirikiana na mahakama mfano mzuri ni Mawakili wa serikali, mawakili wa kujitegemea, mabaraza ya kata, jeshi la polisi na magereza pamoja na asasi mbalimbali zinazotoa msaada wa kisheria. Kama ilivyoeleza hapo juu mahakama ndiyo inayowajibika kimsingi katika utoaji haki.

## DHANA YA MAADILI

Mheshimiwa mgeni rasmi, neno maadili linatokana na neno "Adili" linahusiana sana na mwenendo wa binadamu. "Adili" maana yake ni kuenenda katika usahihi. Maadili ni yale yanayopatikana kwa binadamu yoyote ildhai aweze kutenda kwa uadilifu kadri ya utu wake unaomtofautisha na wanyama, yaani hasa akili inayomwezesha kufikiria na kuelewa maana na matokeo ya matendo yake. Binadamu yoyote ana uwezo wa akili wa kuongoza mawazo yake na matendo yake katika mkondo unaofaa ambao utakuwa na faida kwake na kwa jamii inayomzunguka.

Tafsiri ya maadili ni pana lakini kwa ujumla ni tabia au mwenendo mwema wa mtu katika taasisi au jamii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa umma. Maadili yanahusu tabia na mwenendo unaokubalika katika jamii. Tabia ni mazoea yanayotokana na kurudia hali, mwenendo au matendo. Mazoea

ya hali, mwenendo au matendo yanayolenga katika mambo mema ya haki na usawa ndiyo maadili.

Maadili ya utendaji huweka viwango vya kutambua, kuzuia na kusimamia hali zinazoweza kuleta mgongano. Viwango hivi vinaweza kujumuisha miongoni mwa mengine mwenendo binafsi, uadilifu, usiri, uwajibikaji, uwazi, zawadi, faida, matumizi ya mali za umma, kuwa na kofisa mbili za madaraka na ajira baada ya kustaafu.

**JUKUMU LA MSINGI LA UTOAJI HAKI KWA WAKATI**

Mahakama ya Tanzania inao wajibu wa kutekeleza jukumu la utoaji haki kwa wananchi kwa wakati. Kama ambavyo imeweza kuahinishwa katika ibara ya 107A ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, " mamlaka ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia itakuwa mikononi mwa Mahakama. Na kazi yake kubwa ni kutafsiri sheria zilizotungwa na Bunge. Ibara ya 107A (2) (b) ya katiba hiyo hiyo inaitaka mahakama kuhakikisha inatimiza jukumu lake hilo la utoaji haki kwa wakati pasipo kuchelewesha kesi bila sababu za msingi.

Kutokana na jukumu hilo, mahakama ya Tanznaia, kupitia mahakama zake ambazo ni mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mahakama za Hakimu mkazi/ Mkoa, mahakama kuu na Division zake ( mahakama kuu divisheni ya kazi, biashara, ardhi na mahakama kuu Division ya Makosa ya Rushwa) pamoja na mahakama ya Rufani, zimekuwa zikitekeleza jukumu hili la msingi kw akujiwekea mikakati mbalimbali kuhakikisha kesi zinamalizika kwa wakati.

**MAHAKAMA NA MIKAKATI YA KUMALIZA KESI KWA WAKATI**

Mahakama ya Tanzania imejiwekea mpango mkakati wa kuhakikisha mahakama zote za Tanznaia kuanzia mahakama za mwanzo, wilaya, mahakama ya hakimu mkazi pamoja na mahakama kuu na division zake. Zinamaliza kesi katika kipindi ambacho wamejipangia. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano unaotekelezwa katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2019/2010. Mpango huu ni dira na mwelekeo wa mahakama katika kufikia lengo lake la kuwa mahakama iliyokaribu na inayofikiwa na wananchi kw aurahisi katika kutoa huduma bora za utoaji haki. Aidha mpango mkakati huu unalenga kufikia malengo ya dira ya maendeleo ya Tanznaia ya mwaka 2025 ya kuifikisha nchi kwenye uchumi wa kati.

Ili kutekeleza suala la kumaliza kesi zilizopo mahakamani kwa wakati, mahakama ya Tanznaia, imepanga muda maalum wa kumaliz akesi katika mahakama zake mbalimbali, kwa mfano, katika mahakama kuu, kesi inatakiwa kumalizika ndnai ya kipindi cha miaka miwili, mahakama za mikoa na wilaya, kesi zinatakiwa kumalizika ndnai ya miezi kumi na miwili, wakati kwa mahakama z amwanzo kesi zinatakiwa kusikilizwa na kumalizika ndnai ya miezi sita tu.

Katika uzingatiaji ukomo wa muda, mahakama imefanikiw akwa kiwango kikubwa hasa kw amahakama za mwanzo ambazo zinachukua asilimia zaidi ya 70% ya mashauri yote mahakamani. Kwa mahakama za mwanzo za Morogoo zimefanikiwa kwa kiwango cha asilimia 99% kaika kumaliza mashauri yote kwa mwaka 2016/2017. Hakuna kesi ambayo utaikuta mahakama ya mwanzo yenye umri wa miezi sita na kuendelea kwa mahakama za mwanzo Mvomero. Kwa mahakama za Wilaya na mahakama ya hakimu mkazi, zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuondokana na mlundikano wa mashauri ya muda mrefu. Isipokuwa kwa mashauri yale ambayo mahakama hizi hazina mamlaka nayo.

Mkakati mwingine uliowekwa na mahakama ili kumaliza kesi kwa wakati, ni ule wa kufanya vikao na wadau ili kujadili namna ya kumaliza kesi kwa wakati kwa kuwa kitendo cha kuchelewa kwa kesi hakisababishwi na mahakama pekee bali wadau wa mahakama pia wanahusika. Wadauo hawa ni pamoja na mawakili wa serikali kupitia ofisi ya mwanasheria Mkuu wa serikali pamoja na Kurugenzi ya Mashtaka, Mawakili wa kujitegemea, jeshi la polisi kupitia wapelelezi wa mashauri ya jinai na asasi mbalimbali zinazotoa msaada wa kisheria kwenye makundi maalum au kwa wananchi kw aujumla. Hii yote ni jitihada ambayo mahakama imekuwa ikiifanya ili kuhakikisha kuwa inashirikisha wadau wake wanaokuwa nao katika uendeshaji wa mashauri husika. Hii yote ni kuhakikisha kwamba kila muhusika anatimiza wajibu wake kama inavyotakiwa ili kesi ziweze kumalizika kwa wakati uliopangwa.

Mpango mkakati wa mahakama wa miaka mitano, unazingatia nguzo tatu za utawala bora na menejiment ya rasilimali na upatikanaji na utoaji wa haki kwa wakati na kuimarisha imani ya jamii na ushirikishaji wa wadau. Ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wakati, Majaji na mahakimu wamejipangia mikakati kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwa na idadi maalum ya kesi ambazo wanatakiwa kumaliza kwa mwaka, mfano Majaji wa mahakama ya rufani na mahakama kuu ya Tanznaia wanatakiwa kusikiliza na kumaliza kesi 220 kwa mwaka, huku mahakimu wa mahakama za Hakimu mkazi na Wilaya wanatakiwa kusikiliza na kumaliza kesi 250 kwa mwaka, kwa mahakimu wa mahakama za mwanzo wanatakiwa kumaliza kesi 260 kwa mwaka.

Mheshimiwa mgeni rasmi, mahakama ya Tanznaia imekuwa katika mpango wa kuboresha huduma, imeweza kuhakikisha kwamba inatoa huduma bora kwa wananchi, hasa hasa katika jukumu lake la msingi la utoaji haki kwa wananchi wote wanaoitafuta haki hiyo

katika mahakama zetu zote, kuanzia mahakama za mwanzo hadi za rufani. Ubunifu mbalimbali umefanyika ili haki hizo ziweze kupatikana kwa wakati. Hii yote ni kumuwezesha mwananchi kuendelea na shughuli zake binafsi ili kuweza kukuza uchumi wake pamoja na wa Taifa. Nina uhakika kabisa kama wananchi wanafatilia shughuli za Mahakam, watakubaliana na mimi kwamba mabadiliko makubwa sana ya utendaji kazi yanazidi kuonekana kwa mahakama kila mwaka. Mashauri mengi yameweza kumalizika kwa wakati ambao mahakama imejipangia ili kupima utendaji kazi wenye ufanisi na kuleta tija kwa wananchi wote wanaohitaji huduma hii. Kwa kifupi mahakama za mwanzo za Wilaya ya Morogoro na Mvomero zimeweza kumaliza mashauri yote ya mwaka 2017 na kuweka kumbukumbu ya zero pending (mashauri sifuri) na mahakama nyingine z amwanzo zikiwa zimefanikiwa kumaliza mashauri kwa kiwango cha asilimia 95. Mahakama ya Mvomero kwa asilimia 95 hakimu mkazi zimejitahidi kwa kiasi kikubwa kumaliza kesi zenye mlundikano, na kesi nyingi ambazo zimebaki za kuanzia 2018 kushuka chini ni kesi zile tu ambazo mahakama hizi hazikuwa au hazina mamlaka ya kusikiliza. Kesi hizi ni pamoja na mashauri mauaji, madawa ya kulevya, pamoja na uhujumu uchumi.

**DHANA YA MAADILI**

Mheshimiwa mgeni rasmi, neno maadili linatokana na neno “Adili” linahusiana sana na mwenendo wa binadamu. “Adili” maana yake ni kuenenda katika usahihi. Maadili ni yale yanayopatikana kwa binadamu yoyote ildhai aweze kutenda kwa uadilifu kadri ya utu wake unaomtofautisha na wanyama, yaani hasa akili inayomwezesha kufikiria na kuelewa maana na matokeo ya matendo yake. Binadamu yoyote ana uwezo wa akili wa kuongoza mawazo yake na matendo yake katika mkondo unaofaa ambao utakuwa na faida kwake na kwa jamii inayomzunguka.

Tafsiri ya maadili ni pana lakini kwa ujumla ni tabia au mwenendo mwema wa mtu katika taasisi au jamii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa umma. Maadili yanahusu tabia na mwenendo unaokubalika katika jamii. Tabia ni mazoea yanayotokana na kurudia hali, mwenendo au matendo. Mazoea ya hali, mwenendo au matendo yanayolenga katika mambo mema ya haki na usawa ndiyo maadili.

Maadili ya utendaji huweka viwango vya kutambua, kuzuia na kusimamia hali zinazoweza kuleta mgongano. Viwango hivi vinaweza kujumuisha miongoni mwa mengine mwenendo binafsi, uadilifu, usiri, uwajibikaji, uwazi, zawadi, faida, matumizi ya mali za umma, kuwa na kofisa mbili za madaraka na ajira baada ya kustaafu

**KUIMARISHA UWAZI NA KUZINGATIA MAADILI**

Mheshimiwa mgeni rasmi, mahakama ya Tanzania kwa hivi sasa ipo kwenye mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba inafikia kiwango bora nchini kwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, weledi na ubunifu ili kuwawezesha wananchi kupata huduma za kimahakama kwa njia ya mtandao katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha kuwa wanaondoa malalamiko yanayotokana na utoaji wa huduma usiokidhi viwango. Hakuna ubishi kabisa kwamba watumishi wa mahakama wa kada zote wasipotimiza wajibu wao kikamilifu wanasababisha malalamiko kwa wananchi na kuifanya mahakama kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea. Na haki hii inafanya wananchi kuwa na imani ndogo na mahakama. Lakini kupitia taarifa zetu kwenye mtandao itahimarisha imani ya wananchi kwa mahakama kwani taarifa watakuwa wanazipata kwa urahisi na haraka sana kila watakapohitaji kuziona na kuzipata.

Mheshimiwa mgeni rasmi, kanuni za maadili za utendaji kazi zinaundwa kw akutarajia au kuzuia aina Fulani za tabia kwa mfano, migongano ya maslahi, kujinufaisha binafsi, rushwa na vitendo vya uvunjifu wa maadili. Hatua zinazochukuliwa kusimamia maadili zinapaswa kuwa na nyenzo za kuzuia tabia

ambazo zinaonekana kuwa mbaya, kuhamasisha mwenendo unaoonekana kuwa sahihi na kuhakiki masuala ambayo hayana uhakika wa kimaadili. Kwa kawaida hii inafuata mfumo wa tunu au kanuni za maadili.

Mheshimiwa mgeni rasmi, Tuhuma au malalamiko mengi ya makosa, kashfa au uvunjaji wa maadili ni kutokana na tabia zisizo za kimaadili kwa baadhi ya watumishi wa mahakama ambao hukiuka sheria na kanuni kwa hiyo jitihada za kuzuia rushwa kw awatumishi wa mahakama na lugha ambazo siyo sahihi, lazima ziwe na mfumo wa kuzuia vitendo visivyo vya kimaadili na kuhamasisha mwenendo unaoonekana kuwa sahihi na kuhakiki masuala ambayo yanaonekana kutokuwa na uhakika wa kimaadili kwa njia ya maelekezo ya njia sahihi ya kufuata inaweza kutazamwa kama usimamizi wa maadili kwa kutumia tunu (value based).

Tumeona juhudi mbalimbali zikifanyika kuhakikisha kwamba watumishi wa mahakama wanakuwa na tabia na mwenendo unaokubalika kwa jamii ili kuongeza imani kwa wananchi katika muhimili huu muhimu wa utoaji haki. Suala la uadilifu linatiliwa mkazo kwa vitendo. Tuna kamati za maadili ngazi ya Wilaya na mkoa. Hizi zinahusika moja kw amoja na mahakimu ambao wamelalamikiwa kuwa na kashfa za utovu wa nidhamu au uvunjaji wa maadili. Kwa mahakimu wa mahakama ya mwanzo wanaitwa katika ngazi ya Wilaya kuhojiwa mwenyekiti akiwa Mkuu wa Wilaya na wajumbe wengine. Hivyo hivyo anayekiuka maadili kuitwa na kuhojiwa katika kamati ya maadili ngazi ya Mkoa. Mwenyekiti akiwa Mkuu wa Mkoa na wajumbe wengine.

Lakini kama hiyo haitoshi, tumekuw ana vikao vya ndnai vya mara kwa mara kusisitiza maadili kwa watumishi wa mahakama katika kada zote.

Pia tumeanzisha kamati za nidhamu katika kila mahakama kuanzia mahakama zetu za mwanzo, wilaya na mahakama ya hakimu mkazi katika Mkoa wa Morogoro. Kupitia dawati la

malalamiko ambapo anakuwepo afsa wa kupokea malalamiko kwa kushughulikia yale ambayo yapo ndnai ya uwezo wake. Yale yanayomshinda kuyafikisha kw akiongozi husika na kushughulikiwa mara moja.

Pia ufanyaji wa malipo benki kwa ada za mahakama na malipo yoyote yale yanayohusiana na faini ya mashauri mbalimbali, hii yote ni kuepusha ubadhirifu wa fedha ambao uliokuwa ukijitokeza sana kwa baadhi ya watumishi wa kada ya uhasibu na makarani ambao wamekuwa wakifanya kai hiyo kw akukiuka maadili ya kazi yao. Wapo waliochukuliwa hatua ya kufukuzwa kazi kutokana na kashfa hizo lakini pia wapo ambao mpaka sasa wamesimamishwa wakipisha uchunguzi uendelee.

Pia uvaaji wa vitambulisho vyenye jina la mtumishi husika na namba katika sare zetu za ofisini. Hii yote ni kuhakikisha maadili yanazingatiwa. Na kwa mtumishi yeyote Yule atakayekiuka kwa kutoa lugha isiyofaa kwa mteja wa mahakama au kuomba rushwa, basi inakuwa rahisi kwa mteja huyo kumripoti kwa kiongozi wake.

Sambamba na hilo mabango mbalimbali ya kupambana na rushwa yamebandikwa katika mahakama zote za Mkoa wa Morogoro na mabango mengine kusambazwa sehemu mbalimba ili tu wananchi waweze kuona na kusaidia kutoa taarifa za uvunjifu wa maadili haraka zinapojitokeza. Mabango yana namba za simu za kupeleka malalamiko yao pindi tu wanaposhawishiwa kutoa rushwa au kujibiwa kwa lugha zisizofaa, kuzungushwa bila sababu za msingi katika kujipatia nakala ya hukumu.

Pia majaji na mahakimu wamekewa idadi ya mashauri ya kumaliza kwa kila mwaka, muda wa kutoa hukumu na mwenendo, hii yote ni kuhakikisha kuwa kila mmoja anafanya kazi yake ipasavyo na kw auadilifu mkubwa.

Utafiti wa kileo wa saikolojia ya kijamii unaonyesha kwmaba kanuni za maadili zinaweza kuongoza au kushawishi tabia katika nchi zinazoendelea ambazo ni muhimu kwa utumishi wa

mahakama uliotukuka. Kanuni za maadili zinaweza kuwa na athari chanya kwa tabia ya watu wabaya katika taasisi, unaweza pia kuzitambua na kuchukua hatua kuzirekebisha. Pia watu mara nyingi husita kufanya kitendo kiovu ikiwa wanaamini kwmaba kila mtu anayewazunguka anajua kuwa hicho ni kitendo kiovu. Aidha watu wanajihusisha na vitendo vya rushwa wanaamini kuwa wanaweza kukamatwa wanapokuwa katika mazingira ambayo yanasisitiza tabia ya kimaadili. Tabia ya maadili inapaswa kuwa mazoea kwa watumishi wa mahakama. Hii inaongeza ufanisi na kuweka viwango vya maadili ambavyo vinawawezesha watumishi wa mahakama kupima matendo yao kutokana na viwango vya maadili vilivyowekwa. Pia watumishi kuwa na utayari wa kutoa huduma kwa wananchi kw akuzingatia viwango vya maadili.

## KANUNI ZA MAADILI AMBAZO WATUMISHI WA MAHAKAMA WANATAKIWA KUZIFUATA

1. Kutokuwa mbinafsi; watumishi wa mahakama wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maslahi mazima ya wananchi. Hawapaswi kufanya jambo ili kujipatia manufaa ya kifedha au manufaa mengine kwao wenyewe, familia zao au marafiki zao.
2. Mahakimu wenye dhamana katika utoaji haki mahakamani hawapaswi kujiweka chini ya wajibu wowote wa kifedha au wajibu mwingine kwa watu binafsi au taasisi ambazo zinaweza kuwashawishi katika utendaji wa kazi zao.
3. Mahakimu kutopendelea upande wowote ule katika maamuzi mbalimbali ya kesi zinazoletwa mahakamani. Kuhakikisha kila upande unapata kile unachostahili.
4. Uwajibikaji, watumishi wa mahakama wote wana wajibu wa kuwajibika kila mmoja katika nafasi na kutekeleza wajibu wao bila kuomba au kushawishi kupewa pesa au chochote kile ambacho siyo haki yake kukipata katika utekelezaji wa majikumu hayo kutoka kwa wadaawa wa mahakama

5. Uwazi viongozi wa mahakama wanapswa kuwa wawazi kadri iwezekanavyo kuhusu maamuzi na hatua zozote wanazochukua kwa watumishi ambao wanaenda kinyume na maadili ili watumishi wengine wajifunze kupitia hao watakaokuwa wamechukuliwa hatua.

Mahusiano baina ya watumishi na wateja wa mahakama yatajengwa na kuboreshwa kama tu watumishi w amahakama watakuwa na maadili na kudhibiti tabia zao na mawazo yao katika mkondo unaofaa. Ili mahakama iendelee kuaminiwa na wananchi uwazi na maadili ni jambo la msingi sana. Hatuwezi kuifikia mahakama yenye haki kw akiwango bora ziaid bila kuwa na maadili kwanza. Ni lazima watumishi wa mahakama waangaliwe kw aukaribu kuhakikisha kwamba wana maadili na wanafanya kazi kwa uadilifu mkubwa. Ilikujenga mahakama imara na kufikia malengo ya utoaji haki kwa wakati na kwa anayestahili basi uzingatiwaji w amaadili lazima upewe kipaumbele. Hivyo basi watumishi w amahakama wanawajibika kubadilika na kuwa na mtazamo chanya na kuongoza mawazo yao katika mkondo unaofaa.

Ni ukweli usiopingika kwamba bado kuna baadhi ya wananchi hawana imani na mahakama. Na hii imesababishwa na baadhi ya watumishi wa mahakama ambao wamekosa uadilifu. Ili kurudisha imani ya wananchi kwa mhimili huu watumishi hao wachache wanaoitia doa mahakama wanatkiwa kubadilika na kubadilisha mwelekeo wa mawazo yao na tabia zao pia.

## CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO

Mhe, mgeni rasmi pamoj an ajitihad azote hizo za kuboresha huduma katika mahakama zetu, mahakama ina malengo ya kujenga mahakama za mwanzo katika kila kata, mfano katika wilaya yetu, kuna kata ambazo zipo mbali na huduma ya mahakama, kata hizo ni pamoja na Kinda, Dakawa, Maskati, Pemba, Mkindo na kibati.

Mhe, mgeni rasmi jukumu la kujenga majengo ya mahakama sio la mahakama peke yake, pia ni la wananchi katika eneo husika, halmashauri ya wilaya n amahakama yenyewe. Hivyo tunatoa wito kwa wananchi wakishirikiana na serikali za mitaa kutenga maeneo ya ujenzi wa Mahakama na kuanzisha ujenzi wa mahakama ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za mahakama kwa wakati (mfano ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo - Mvomero ulianzishwa na wananchi wenyewe)

Mhe, mgeni rasmi tunatambua kuwa wewe unalo jukwaa la kuongeana wananchi pamoja na watendaji wako wa serikali za mitaa, hivyo tunakuomb autufikishie salamu zetu kwa wananchi juu ya ujenzi wa mahakama katika sehemu mbalimbali ndani ya wilaya yetu ili kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi.

Mhe, mgeni rasmi pamoja na jitihada za mahakama kutekeleza majukumu yake, tuna changamoto kadhaa kama ifuatavyo;

1. Hatuna jengo la kudumu la Mahakama ya / wilaya hata hivyo tunakushukuru kwa kutupatia ofisi katika jengo lako.
2. Hatuna nyumba zaWaheshimiwa mahakimu
3. Upungufu wa vitendea kazi mfano computer
4. Mahakama ya wilaya haina gari maalumu ya kufanya shughuli mbalimbali za kimahakama ikiwemo ukaguzi wa mahakama za mwanzo.

Mhe, mgeni rasmi, endapo utapata wafadhili au mfuko wa ofisi yako utakapo ruhusu, usisite kutusaidia kutatua changamoto hizo.

Ni ukweli usiofichika kwamba hadi sasa kuna baadhi ya mahakama za mwanzo ambazo hazina umeme na pia miundo mbinu yake inakuwa ni migumu kwa umeme kuweza kufika. Hivyo basi ili matumizi haya ya TEHAMA yaweze kurahisisha shughuli za mahakama na katika ubora unaotakiwa, hakuna budi kwa

mahakama zote za mwanzo ambazo hazina umeme, ziweze kufikishiwa huduma hiyo ili kuendana na dira ya mahakama. Kwani kwa kufanya hivyo vitendea kazi vitaweza kupelekwa na kuunganishwa katika mtandao. Hali hii itafanya hata taarifa za mahakama hizo ziweze kuingiza kwenye mtandao kirahisi badala ya kusubiria mpaka ziletwe mawilayani kwa ajili ya kuziingiza kwenye mtandao.

Pia ukiangalia katika dira ya mahakama, mkakati uliopo ni kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano unaotekelezwa katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2019/2020. Mpango huu ni dira na mwelekeo wa mahakama katika kufikia lengo lake la kuwa mahakama iliyo karibu na inayofikiwa na wananchi kwa urahisi katika kutoa huduma bora za utoaji haki. Lakini mpaka sasa mahakama ya Wilaya ya Mvomero bado haijajengwa. Yote hii inasababishwa na ufinyu wa bajeti hata hivyo jitihada za kutafuta fedha za ujenzi zinafanywa.

**HITIMISHO.**

Ndugu mgeni rasmi, ninapo hitimisha vilevile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Ofisi yako na Mkurugenzi kwa kuhakikisha huduma hii ya Mahakama ya Wilaya ya Mvomero inatolewa ndani ya Wilaya hii na pia kufanikisha shughuli hii ya wiki ya sheria mpaka kufikia leo siku ya kilele. Pia ninakushukuru kwa kuitikia wito huu wa kuungana nasi katika maadhimisho haya muhimu, pia tunawashukuru viongozi waliohudhuria katika sherehe hizi, pamoja na wananchi wote, ahsanteni sana kwa kunusikiliza na karibuni tena katika maadhimisho yajayo.